Catholic Diocese of Tanga
Hills View English Medium School
Magunga District Hospital Road
Mob:+255 -784808420, +255 718 661681 , +255 714901004
www.rmet.ac.tz, email: saroce2013@gmail.com
**KOROGWE, TANZANIA**

Kumb
.Na.HVEMS/JI/DT/018 Novemba 17, 2017.

Mpendwa Mzazi /Mlezi wa ________________________________

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE CHINI YA TAASISI YA ROCK MEMORIAL EDUCATION TRUST 2018**

Ninafurahi kukujulisha kuwa mwanao…………………………………………………amechaguliwa na Baraza la Taaluma la Taasisi ya Rock Memorial Education Trust kujiunga na:

- ✓ **Darasa la……………….katika Shule yake ya Mchepuo wa Kiingeraza Hills View.**
- Kidato cha I katika shule yake ya Sekondari Hill View – Bweni/ Mchanganyiko
- Kozi ……………………………katika Chuo chake cha Elimu ya Awali cha Mt. Rock

1. **Shule ilipo:**
Tupo km 2 ½ kutoka stendi mpya ya mabasi Kilole pembeni mwa barabara iendayo hospitali ya Wilaya Magunga au Kwamgoma. Mwambie kondakta akushushe CRDB na NMB bank. Unaweza kufika kwa bajaji sh. 1,000/= au pikipiki sh.1000/=

2. **Afya:**
Mtoto apimwe afya na daktari na kumjazia Fomu Na. CHRS iliyoambatanishwa na kuirejesha kwa Msajili kabla au siku ya kuripoti.

3. **Kuripoti Shuleni:**
Mtoto aripoti Jumamosi tarehe 08, Januari kuanzia saa 1:30 asubuhi akiwa nadhifu na kila mtoto aletwe na Mzazi, Mlezi au Mfadhili wake. Atakayechelewa siku 3 baada ya tarehe 6, Januari atalipa tozo la usumbufu la shs. 10,000/=.

4. **Ada :**
Gharama za Elimu na Malezi kwa mwaka wa kwanza wa masomo ni ‘Baby’ Tshs. 120,000/= ‘Nursery’ Tshs. 240,000/= na ‘Pre-school’ Tshs. 300,000/= kwa mwaka wa masomo wote.

Jedwali lifuatalo laweza kukuongoza ingawa halizuii mfumo wa ulipaji kwa mikupuo.

| Awamu za ulipaji kwa mwaka 2018 | | | |
|---|---|---|---|
| **Darasa** | **Jan** | **Mei** | **Agosti** |
| **Baby** | **50,000/=** | **40,000/=** | **30,000/=** |
| **Nusery** | **120,000/=** | **80,000/=** | **40,000/=** |
| **Pr. School** | **120,000/=** | **100,000/=** | **80,000/=** |

Malipo yote yafanywe kwa Mmiliki :- Rock Memorial Education Trust A/Cs 41503500031 NMB au OIJ1098887200 CRDB au TIGOPESA namba ya Kampuni 757575 na mlete mwanao na "Original Pay in Slip" yenye jina lake na darasa ili apewe stakabadhi. Ada ikishapokelewa hairudishwi.

5. **Mchango wa Usafiri wa Watoto:**
Mwenendo wa usafirishaji umekuwa ukitoa taswira ya ubaguzi zaidi kuliko usawa na ili kukabiliana na hali hii, mzazi itampasa achangie Tshs. 10,000/= kila mwezi kwa ajili ya usafiri wa mtoto wake.

**6. Sare:**
Mtoto aandaliwe na sare 2 za darasani (Brown na Cream) Isteem No. 1" na 2 za kushindia kama sampuli ya vitambaa ilivyoambatishwa. Tshirt sh. 10,000/= na Sweta sh. 15,000/=, vinapatikana hapa shuleni . Sare zote zifumwe vizuri majina ya mtoto kwa uzi. Sketi za wasichana ziwe inch 5 kutoka kwenye magoti.

**7. Ratiba ya Mikutano ya wazazi katika mwaka:**
Ili kuwa na mfumo imara wa ushirikiano kati ya shule na wazazi mwaka 2018 tumetaka tuzingatie yafuatayo:-
- Mikutano ya wazazi tarehe 13/01/2018 na wa pili tarehe 08/09/2018.
- Mikutano hii ni muhimu, kwani ni ya kimalezi kwa maendeleo ya kitaaluma ya watoto wetu, kila mwezi analazimika kuhudhuria.

**8. Mwisho:**
Ni matumaini ya uongozi wa shule hii kwamba utayazingatia maelekezo haya ili kupunguza usumbufu kwa maendeleo ya taaluma na malezi ya mwanao na kuwatakieni sikukuu njema ya Christmas mwaka mpya wa 2018.

Karibu Hills View,

**C. Mhuza**
**Mkuu wa Shule**

**Nakala:** Meneja wa Shule
Hills View English Medium School

Catholic Diocese of Tanga
# Hills View English Medium School
Magunga District Hospital Road
Mob:+255 -784808420, +255 718 661681 , +255 714901004
www.rmet.ac.tz, email: saroce2013@gmail.com
**KOROGWE, TANZANIA**

Tafadhali jaza fomu hii na uirejesha kwa msajili siku ya kumleta.
Weka alama (V) kwa Mafunzo unayoomba: Baby ( ); Chekechea ( ); Awali ( ); Darasa la ( )

1. Majina matatu kamili ya mtoto …………………………………………………………Drs………. Mwk…..

2. Tarehe ya kuzaliwa ………….Namba ya cheti cha kuzaliwa …………. Mahali alipozaliwa……..

3. Jina la Baba/Mama/Mlezi ……………………………………………………………………………………….

4. Kazi yake………………………Kijiji/Mtaa……………….Kata……………………. Wilaya…………………….
   Anuani ……………………………………… Simu ya ofisini……………………… Simu Kiganjani…………..
   Barua Pepe……………………………… Simu ya ndugu wa karibu……………………………
   Uraia…………………………………………Dini…………………..

5. Taarifa ya afya ya mtoto: Ijazwe na Daktari, kuzingatia maradhi haya:
   Donda koo……………Pepo punda…………..Kisukari…………Kifafa……………Kifua kikuu………
   Mapunye………….. Meno……………Ukojozi……………… Minyoo……………Pumu…………………
   Vidonda tumbo: ……………………Hernia……………..na ugonjwa mwengine…………………………

6. Mtoto ana mzio (allergy) au ugonjwa mwingine:
   Eleza: ………………………………………………………………………………………………………………

   Mtoto wako anatumia matibabu nyumbani? Ndiyo/Hapana kama ndio ni aina gani ya dawa (tiba)……………………………………………………………………………………………………………

   Mtoto wako akiugua Malaria ni dawa gani humtibu? ……………………………………………………

   Jina la Daktari……………………………………saini…………………Mhuri…………………Tarehe…………

7. Uthibitisho: Mimi……………………………………………………Baba/Mama/Mlezi wa …………………
   Nathibitisha kwamba kama mwanangu atajiunga na shule hii nitashirikiana kwa karibu na uongozi wa shule katika kustawisha taaluma na maadili ya mtoto wangu. Nitakubaliana na kanuni na sheria za shule na kulipa kwa wakati kama itakavyoelekezwa mara kwa mara.

   JinaBaba/Mama/Mlezi……………………………………………saini…………….tarehe……………………

   Mwalimu Mkuu…………………………………………………saini…………………tarehe……………………